# MINUTE SHEET

| DOKEZO No. | |
|---|---|
| 11 | KITENGO CHA ARDHI F.27<br>Insignia Ltd, imewasilisha maombi ya kuongeza Plot No. 169 APT No. 10C, (Apartment) iliyopo Upanga, Dar es Salaam kwaajili ya makazi ya wakurugenzi wa kampuni ya Insignia Ltd.<br>Insignia Ltd ni ~~mra~~ kampuni iliyosajiliwa na Kituo na kupata cheti cha Uwekezaji No. 04024902 kwaajili ya kutekeleza mradi wa Kiwanda cha kutengeneza Rangi, vifungasho vya bidhaa asili ya vyuma na vifungasho vya plastic.<br>Kwa maelezo hayo, tunaomba mwongozo, kwa Kisheria, Kanuni na Taratibu za umilikishwaji wa "Unit Tittle" kwa wageni ambao ni wamiliki wa mradi tajwa.<br>Nkrma.<br>IFO 12/10/2021 |
| 12. | IFO<br>M. 11<br>Kwa mujibu wa sheria mwekezaji anaruhusiwa kununua Appartment Kama ni sehemu ya uwekezaji wake. Hii Inawezekana tu Kama mradi uliosajiliwa TIC unatekelezwa Ipasavyo. Appartment Kama Ipo kwenye mfumo wa Unit TIC itanunua kwenye niaba ya mwekezaji baada ya Milki kuhamia TIC utaratibu wa kutoa Derivative Right kwa mwekezaji utafuatwa kwa mujibu wa sheria.<br>LO<br>JHau.<br>12/10/2021 |